

TARATIBU ZA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA AFYA

1.0 UTANGULIZI

1.2 Utaratibu wa kushughulikia masuala ya nidhamu katika Utumishi wa Umma kwa makosa makubwa (*Formal Proceedings*) ambayo kama mtuhumiwa atapatikana na hatia anaweza kufukuzwa kazi kuteremshwa cheo/madaraka pamoja na kupunguzwa mshahara umeelezwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, **Kanuni za 47 na 48.**

2.0 MCHAKATO WA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU

Kwa ufupi Kanuni zinaelekeza kwamba:-

1. Mtumishi akituhumiwa kwa kosa lolote kubwa, Mamlaka yake ya Nidhamu inapaswa kufanya kwanza uchunguzi wa awali ili kujiridhisha kama kweli kosa limefanyika na kuna haja ya kumfungulia mtuhumiwa mashataka. *Mamlaka za Nidhamu kwa watumishi wa afya ni Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, kwa wale walioko Wizarani au katika vyuo na taasisi za afya, Katibu Tawala wa Mkoa, kwa watumishi wa Hospitali ya Mkoa na Mamlaka ya Halmashauri kwa watumishi wa Halmashauri.*
2. Kama itaonekana mtumishi anazo tuhuma za kujibu, basi Mamlaka ya Nidhamu iandae Hati ya Mashtaka na Notisi na kumpa mtuhumiwa.
3. Endapo Mtuhumiwa atakiri kosa, Mamlaka ya Nidhamu itatoa adhabu inayohusika.
4. Endapo atakana tuhuma basi Mamlaka ya Nidhamu itaunda Kamati ya uchunguzi.

5. Kamati ya uchunguzi itamjulisha mtuhumiwa tarehe, muda na mahali uchunguzi utakapofanyika.
6. Mtuhumiwa atakuwa na haki ya kupewa nyaraka zilizotumika kama ushahidi kuwakilishwa na wakili au mtumishi mwingine kama akitaka pamoja na kuwahoji mashahidi pamoja ana Mamlaka ya Nidhamu.
7. Kamati ya uchunguzi itatakiwa kukamilisha uchunguzi ndani ya siku sitini (60). Kama Kamati itahitaji muda zaidi, Mamlaka ya Nidhamu inaweza kuongeza muda zaidi wa siku 30. Iwapo muda huo wa nyongeza wa siku 30 hautoshi, basi Mamlaka ya Nidhamu itaomba kibali cha kuongeza muda zaidi kutoka Ofisi ya Rais, menejimenti ya utumishi wa Umma.
8. Baada ya uchunguzi kukamilika, Kamati ya uchunguzi itawasilisha taarifa ya uchunguzi kwa Mamlaka ya Nidhamu. Taarifa hiyo itatakiwa kuonyesha endapo mtuhumiwa ana makosa au la na sababu za maoni hayo. Kamati haitakiwi kupendekeza adhabu.
9. Mamlaka ya Nidhamu ikishapokea taarifa ya uchunguzi, itatakiwa kumjulisha mtuhumiwa uamuzi ndani ya siku 30 tangu ipokee taarifa hiyo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 48 (6).
10. Endapo mamlaka ya Nidhamu itashindwa kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa itachukuliwa kuwa mtuhumiwa hana makosa .

3.0 MTUHUMIWA WA MAKOSA YA KITAALUMA

Kwa upande wa Utumishi wa Afya, ikiwa mtumishi aliyesajiliwa na Bodi/Baraza la kitaaluma anatuhumiwa kutenda kosa ambalo ni la kitaaluma (*Professional Misconduct*) kifungu cha 151 cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 kinaelekeza kuwa:-

1. Mtumishi huyo atasimamishwa kazi na shauri lake litapelekwa kwenye Bodi/Baraza husika.
2. Bodi/Baraza husika litafanya uchunguzi na taarifa ya uchugunzi itawasilishwa kwa Mamlaka ya Nidhamu ndani ya siku sitini (60) kuanzia tarehe ya kuanza uchunguzi.
3. Kwa kuzingatia taarifa ya uchunguzi, Mamlaka ya Nidhamu inaweza kumfungulia mtumishi husika mashtaka ya Nidhamu kwa kuzingatia Kanuni ya 47-48 kama ilivyokwisha elezwa awali.